Taarifa kwa Vyombo vya Habari
Imezuiwa hadi tarehe 7 Agosti, 2013 saa 5 asubuhi

Watu maarufu wazibwaga sera
Lakini wananchi wanataka kupata data zaidi

7 Agosti 2013, Dar es Salaam: Karibu wananchi wote (97%) wanatambua picha ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ila ni wachache wanaoweza kuelezea kuhusu sera ya MKUKUTA (7%) au Visheni ya Maendeleo ya 2025 (5%). Sera maarufu ya kitaifa inayojulikana zaidi ni Kilimo Kwanza ambapo walau watu 3 kati ya 10 (33%) wamewahi kuisikia na wanaweza hata kuielezea. Baada ya Rais Kikwete, asilimia iliyo chini ya nusu (48%) ya wahojiwa, wanaweza kumtambua Waziri Mkuu Mizengo Pinda. Wakati huo huo, karibia nusu (42%) ya wananchi wangependa Serikali iweke hadharani data na taarifa nyingi zaidi.

Haya ni matokeo yaliyotangazwa na Twaweza kupitia muhtasari wa utafiti unaoitwa *Wananchi, redio, mbao za matangazo: Mahitaji na upatikanaji wa Taarifa nchini Tanzania.* Muhtasari huo umejikita katika data kutoka kwenye utafiti wa *Sauti za Wananchi*, ambao ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanywa kwa njia ya simu za mkononi katika kaya mbalimbali kote nchini Tanzania.

Uamuzi wa Serikali wa hivi karibuni wa kuhama kuelekea kwenye urushaji matangazo ya televisheni kwa njia za digitali na kodi mpya ya kadi za SIM vimeibua mjadala wa kitaifa kuhusu upatikanaji wa taarifa na mawasiliano. *Sauti za Wananchi* ilitaka kujua ni njia zipi za awali Watanzania huzitumia ili kupata taarifa na ni za aina gani; endapo wananchi walikuwa wanawajua wanasiasa na sera; na kama kuna mahitaji ya taarifa kutoka Serikalini.

Redio imeendelea kutawala kama chanzo kikuu cha taarifa na burudani. Wananchi wengi (81%) walithibitisha kuwa wamesikiliza redio ndani ya kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Kati ya hawa, 64% walitumia redio kama chanzo cha taarifa na habari; na 59% waliitumia kwa ajili ya burudani. Katika utafiti huu, karibu wananchi wote (98%) walikuwa wametumia simu za mkononi katika miezi mitatu iliyopita, ila ilibainika kuwa idadi iliyo chini ya 10% walitumia simu ya mkononi kwa ajili ya burudani au habari. Kwa minajiri ya kupata taarifa na habari, baada ya redio, kupashana habari kwa mdomo ndio njia inayofuatia iliyo maarufu ambapo 12% wanapata taarifa na habari kwa njia hii. Hata hivyo, linapokuja suala la utoaji huduma, watu wengi hutaka watoa huduma wa Serikali ndio watumike: utafiti ulionyesha kuwa kwa ushauri wa tiba, 36% wangesikiliza redio wakati 25% wangewauliza wafanyakazi katika zahanati, na kama wangetaka kujua kuhusu shule iliyo bora katika wilaya yao, 33% wangesikiliza redio wakati 29% wangemuuliza mwalimu mkuu au mwalimu mwingine yeyote.

Kama inavyotokea mahala pengi duniani, watu wanakuwa wepesi kutambua wanasiasa maarufu lakini ni wachache tu wanaoweza kuelezea sera muhimu za kitaifa. Kwa ujumla, Watanzania 8 kati ya 10 (81%) wanajua Mbunge wao anaitwa nani, hii ikiwa hasa kwa kiwango cha juu katika maeneo ya vijijini ambako karibu watu 9 kati ya 10 (88%) wanawajua wabunge wao kwa majina. Katika maeneo ya mjini, idadi hii ilionekana kushuka hadi kuwa watu 6 kati ya 10 (63%). Robo tatu ya Watanzania hawajawahi kusikia kuhusu Visheni 2025 (mkakati wa kitaifa unaokusudiwa kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati

itakapofika mwaka 2025) na zaidi ya nusu (53%) hawajawahi kamwe kusikia kuhusu MKUKUTA (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini).

Hata hivyo, wananchi walionyesha kuwa wangependa Serikali itoe taarifa zaidi kuhusu mada mbalimbali zikiwemo za elimu (17%), uchumi na maendeleo (13%), katiba (12%) afya na maji (12%). Taarifa zilizo nyingi wanazodai wananchi zinahusu huduma za msingi na kwa wananchi walio wengi, hiki ndicho kiini ambacho Serikali na umma hupeana taarifa. Watanzania walio wengi wametembelea zahanati (82%) na shule (68%) katika kipindi cha wiki nne zilizotangulia. Katika maeneo haya ya kutolea huduma, mbao za matangazo ni chanzo muhimu cha taarifa ingawa hizi kwa mara nyingi zinakuwa hazipo: ni 35% ya shule na 42% ya zahanati zinazoonekana kuwa na mbao za matangazo. Lakini, walipoulizwa kuhusu taarifa za shule ambazo wangependa kufahamu, wananchi waliorodhesha mambo kadhaa ikiwemo mada za mapato na matumizi ikiwa ni pamoja na Fedha za Ruzuku kwa kila mwanafunzi, mada kuhusu walimu na taarifa za wanafunzi, na hata mada za maendeleo katika sekta ya elimu.

"*Wananchi wanataka taarifa zaidi*," alisema Elvis Mushi, Mtafiti wa Twaweza, "*hasa kuhusiana na upatikanaji wa huduma za jamii katika maeneo yao. Hata hivyo, kukosekana kwa mbao za matangazo katika maeneo ya kutolea huduma hizo kunamaanisha kwamba utoaji taarifa si jambo linalopewa kipaumbele na hakuna mfumo maalumu unaotumika kutoa taarifa, licha ya kanuni na ahadi za Serikali kupitia Mpango wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP .*"

Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisisitiza jambo hilo akisema: "*Kupata taarifa nyingi zaidi ni hitaji ambalo litawasaidia wananchi kushiriki kikamilifu zaidi katika maendeleo ya nchi yetu."*

Muhtasari wa Twaweza unatoa matokeo mengine pia na unapatikana katika mtandao wa Intaneti kwa kwa kiungo hiki: www.twaweza.org/sauti

---- Mwisho ----

Kwa taarifa zaidi:
Risha Chande
Meneja Mawasiliano, Twaweza
Barua pepe: rchande@twaweza.org | **Simu:** (+255) (0) 656 665 7559

Matini kwa Wahariri

- Muhtasari huu na data zake unapatikana kupitia anwani hii ya wavuti www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza ni vuguvugu la miaka 10 lililojikita katika ushiriki wa wananchi, likilenga kuleta mabadiliko makubwa Afrika Mashariki. Twaweza inaamini kwamba mabadiliko ya kudumu yanahitaji uchukuaji hatua kutoka ngazi za chini kwenda juu, na inataka kuibua na kulea mazingira na kupanua fursa ambazo kwazo mamilioni ya wananchi wanaweza kupata taarifa na kuchukua hatua ili kuleta mabadiliko katika jamii zao wenyewe moja kwa moja na kwa kuifanya Serikali iwajibike.
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:
  Tovuti: www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twita:** @Twaweza_NiSisi